


HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA



02/08/2018

TANGAZO LA KUMTAFUTA DALALI WA KUUZA MALI CHAKAVU

1. Halmashauri ya wilaya ya ludewa inategemea kuuza mali zake chakavu ambazo ni magari manne, pikipiki 6, injini chakavu za boti na boti pamoja na vifaa vinginevyo.
 2. Halmashauri inaalika maombi kwa dalali mwenye sifa ili aweze kuuza mali hizo chakavu.
 3. Sifa zinazotakiwa kwa muombaji :-
 - Dalali awe na leseni hai ya udalali
 - Dalali awe ni mlipa kodi na aandike barua yakuonesha kuwa atatoa risiti ya "EFD" wakati wa malipo yake.
 - Kampuni ya udalali iwe imesajiliwa kisheria .
 - Mwombaji aeleze uzoefu alionao katika kufanya kazi hii.
 4. Mwombaji anatakiwa kulipa ada ya maombi ya zabuni fedha taslim Tshs 100,000/= ambazo hazita rudishwa
 5. Mwombaji aeleze utaratibu wa malipo yake utakavyokuwa.
 6. Maombi yatapokelewa kuanzia tarehe ya tangazo hili kuanzia saa 01.30 asubuhi hadi saa 09.30 alasiri kwa siku za kazi tu, mwisho wa kupokea maombi ni jumatano tarehe 15/08/2018 saa 04.00 asubuhi.
 7. Zabuni zitafunguliwa siku ya jumatano tarehe 15/08/2018 saa 04.30 asubuhi katika ukumbi wa Halmashauri ya Ludewa.
 8. Wawakilishi wa makampuni wanaruhusiwa kuhudhuria ufunguzi huo.
 9. Maombi yatumwe kwa anuani ifuatayo :- Katibu Bodi ya Zabuni
- S.L.P. 19 Ludewa


Arch. Ng'wilabuzu N. Ludigiza
Mkurugenzi Mtendaji
LUDEWA
Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya
Ludewa